

Fomu za Kusajili Mikataba inayohusu utajiri wa asili na rasilimali za Nchi iliyosainiwa kati ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wawekezaji

Mwaka 2017 Serikali kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga sheria mbili ambazo ni ***Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Utajiri na Maliasilia za nchi sura ya 449 na Sheria ya Mapitio na majadiliano Kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri na Maliasilia za Nchi, Sura ya 450.***

Sheria hizi zitumike kuweka msukumo katika uangalizi, usimamizi na matumizi ya utajiri wa asili na rasilimali za Nchi ili kuimarisha pato la Taifa na kuwanufaisha wananchi kwa kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii kulingana na matakwa ya vifungu vya 8, 9(i) na 27 vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

Waziri wa Katiba na Sheria kwa mamlaka aliyopewa na Sheria tajwa hapo juu ametunga Kanuni ya ***The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Regulations, 2020*** ambazo zinaweka utaratibu wa kusajili mikataba iliyosainiwa kati ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za serikali, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wawekezaji *kupitia fomu NWR Form - N.1 na NWR Form N.2. Fomu zinapatikana kupitia tovuti ya wizara:* <https://www.sheria.go.tz/publications/51>